



**MZUMBE UNIVERSITY
(CHUO KIKUU MZUMBE)**

TAARIFA MUHIMU KWA WALIOOMBA KUSOMA CHUO KIKUU MZUMBE MWAKA 2017/2018

Chuo Kikuu Mzumbe kinawatangazia wanachuo wote walioomba nafasi za masomo katika programu mbalimbali kuangalia majina ya waliochaguliwa pamoja na taarifa muhimu kuhusu usajili katika tovuti ya Chuo Kikuu Mzumbe www.mzumbe.ac.tz. Mwisho wa wanachuo wote waliochaguliwa kusajiliwa kwa mwaka wa masomo wa 2017/2018 ni tarehe 22 Novemba, 2017 kwa Shahada za Awali na tarehe 28 Novemba, 2017 kwa Shahada za Umahiri.

Ili kupata usajili wa awali, wanachuo wanatakiwa kulipia ada kama ifuatavyo:

- Cheti, Diploma na Shahada ya Kwanza: Tshs. 350,000/=
- Shahada za Umahiri: 800,000/=

Aidha, wanachuo wanatakiwa kulipia kiasi kilichobakia cha ada kabla ya kuanza mitihani ya mwisho ya kumaliza Muhula wa Kwanza kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.

MCHANGANUO WA MALIPO YA ADA KWA MUHULA WA KWANZA

TAREHE MUDA	SHAHADA ZA UMAHIRI	SHAHADA ZA AWALI		
		Shahada za Kwanza za Ualimu, Maktaba, Tehama na Diploma	Shahada za Kwanza Zingine	Cheti
28 Novemba 2017	800,000	350,000	350,000	350,000
31 Disemba 2017	600,000	200,000	200,000	200,000
31 Januari 2018	500,000	174,500	174,500	124,500
15 Februari 2018	540,000	100,000	150,000	100,000

Wanachuo wa ngazi za Cheti, Diploma na Shahada ya Kwanza wenye Bima za Afya zinazotambulika kitaifa, watatakiwa kulipia Tshs. 155,000 ifikapo tarehe 31 Disemba 2017 badala ya Tshs. 200,000.

Wanachuo wa Shahada za Umahiri wenye Bima za Afya zinazotambulika kitaifa, watatakiwa kulipia Tshs. 550,000 badala ya Tshs. 600,000 ifikapo tarehe 31 Disemba 2017. Kwa wanachuo wa Shahada za awali wanaokaa nje ya Chuo, ada yao ya Januari itapungua kwa Tshs. 59,500.

Mchanganuo huo juu wa ulipaji wa ada hauhusishi wanachuo wanaosoma Shahada za Uzamivu (PhD) na Shahada za Umahiri zifuatazo: “MSc. in Health Monitoring and Evaluation, MSc. in Applied Economics and Business, Executive MBA (CM) & Executive

MPA”. Kwa maelezo zaidi kuhusu kozi hizi, wanachuo wawasiliane na Mkurugenzi wa Utafiti, Machapisho na Masomo ya Uzamili (DRPS) na/au Mkuu wa Kampasi ya Dar es Salaam ya Chuo Kikuu Mzumbe (DCC).

Chuo Kikuu Mzumbe pia kinawakumbusha wanachuo wote wanaoendelea kuzingatia kuwa siku ya mwisho wa usajili ni tarehe 22 Novemba, 2017 kwa Shahada za Awali na tarehe 28 Novemba 2017 kwa Shahada za Umahiri.

Imetolewa na:

Kurugenzi wa Mawasiliano

Chuo Kikuu Mzumbe